HUDUMA ZA UPASUAJI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imeendelea kuimarisha huduma bora za upasuaji katika ngazi za Vituo vya Afya (CEmOC) ili kusogeza huduma karibu na wananchi na kupunguza rufaa za kwenda hospitali za wilaya au mikoa



TUFUATILIE KUPITIA ⟶ www.ubungomc.go.tz

UBUNGO FAHARI YETU

HUDUMA BORA

Kwa halmashaui, Vituo vingi vya afya vilivyoboreshwa kama Mpiji Magohe, ambapo sasa vinatoa huduma za dharura za uzazi na upasuaji (CEmOC) kwa akina mama wajawazito wanaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida

Mpaka sasa, Kituo cha Afya Mpiji Magohe kimefanikiwa kutoa huduma za upasuaji 61 kwa mafanikio kuanzia Machi 1, 2026 hadi Oktoba 15, 2026







TUFUATILIE KUPITIA ⟶ www.ubungomc.go.tz

UBUNGO FAHARI YETU

MIUNDOMBIU

Kituo cha Afya Mpiji Magohe, kina Jengo Maalum la upasuaji (theatre), Vyumba vya kufulia na kuhifadhi vifaa vya tiba, Mashine ya kuchemshia na kusafishia vifaa, Maabara, na vyumba vya wagonjwa wa nje na ndani









“Kituo cha afya Mpiji Magohe kinatoa huduma za upasuaji hivyo wananchi wasihofie kuja na kupata matibabu kwa sababu huduma ambazo zinapatikana katika hospitali kubwa, tunafanya kwa ubora”

TUFUATILIE KUPITIA → www.ubungomc.go.tz


UBUNGO yetu
FAHARI YETU


KUPUNGUZA GHARAMA NA MUDA

Wananchi wengi waliokuwa wakisafiri umbali mrefu au kutumia gharama kubwa kufuata huduma za upasuaji mdogo na wa dharura kwenye hospitali za mbali sasa wanahudumiwa Mpiji.

Na halmashauri imehakikisha kunakuwapo Madaktari bingwa katika vituo vya afya kutoa huduma za kibingwa na upasuaji wa magonjwa mbalimbali







TUFUATILIE KUPITIA ⟶ www.ubungomc.go.tz

UBUNGO yetu
FAHARI YETU

UIMARISHAJI HUDUMA

Serikali na Halmashauri imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba na uchunguzi wa magonjwa ili kuweza kutoa tiba stahiki kulingana na ugonjwa.

Hivyo, Uwekezaji huu mkubwa umeleta mabadiliko makubwa katika huduma za uchunguzi wa magonjwa na kupelekea huduma hizi kuwafikia wananchi kwa urahisi katika maeneo wanayoishi na kupunguza usumbufu wa kupoteza muda na gharama za kupata matibabu.



TUFUATILIE KUPITIA ⟶ www.ubungomc.go.tz

UBUNGO FAHARI YETU



Halmashauri ya Manispaa imeandaa jarida hili la utoaji Huduma za Dharura za Uzazi na Upasuaji (CEmOC) kwa akina mama wajawazito wanaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida ili kuuhabarisha Umma wa wana Ubungo juu ya mwenendo wa utoaji wa huduma za afya katika kituo cha Afya Mpiji Magohe.

Kupitia jarida hili, wananchi wa Ubungo watapata uelewa juu ya upatikanaji wa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za Ubingwa na Ubingwa bobezi zinazopatikana katika Zahanati, Vituo vya Afya, na Hospitali. Aidha, Halmashauri itaendelea kutekeleza masuala mbalimbali ya Kisera kama yalivyoainishwa katika jarida hili ili kuendelea kuimarisha afya ya watanzania na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

TUFUATILIE KUPITIA ⟶ www.ubungomc.go.tz

KITUO CHA AFYA MPIJI MAGOHE

Daktari Bingwa Huduma za Upasuaji Mpiji Magohe

DKT. EVANCE MUSHI
Mganga Mfawidhi Kituo cha Afya Mpiji Magohe

Limeandaliwa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Manispaa ya Ubungo



Waandishi

Twagile Sanga
Faraja Mwangata
Rachel Mgeni
Mustafa Mwakibete
Said Sindo
Nasri Mohamed
Lenick Ngao

Mhariri Mkuu

Joina Nzali

www.ubungomanispaa.go.tz